



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA



**TANGAZO LA UJENZI WA VIBANDA MPANDA HOTEL KWENYE MASHINE ZA
MPUNGA ZA ASENGA**


25/03/2024

Halmashauri ya manispaa ya mpanda inakusudia kutumia eneo la mpanda hotel lililopo soko la mahidi jirani na mashine za kukoboa mpunga mkabala na uwanja wa shule ya msingi muungano kwa ajili ya ujenzi wa vibanda 34 vya biashara kwa kuwashirikisha wawekezaji/wadau wa maendeleo mwenye uwezo wa kujenga vibanda kwa makubaliano maalumu.

1. Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda inakaribisha maombi ya wawekezaji wenye nia ya kujenga vibanda vya biashara kuanzia kibanda 01 hadi 34 kulinga na uwezo wake wa kifedha.
2. Mwombaji anatakiwa kupitia mchoro wa vibanda ulioambatishwa kwenye fomu na kisha kujaza gharama atakazo tumia kukamilisha ujenzi wa vibanda hivyo.
3. Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo;
 - i. Awe na uwezo wa kujenga idadi ya vibanda alivyo omba kwa muda wa miezi 05 kwa gharama ambazo muwekezaji atapendekeza.
 - ii. Muombaji aambatanishe bank statement ya miezi 06 nyuma kuanzia tarehe ya Tangazo inayoonyesha uwezo wake kiuchumi.
 - iii. Awe tayari kusimamiwa na wataalamu kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa.
 - iv. Awe tayari kuzingatia viwango vyote vya kitaalamu na kiufundi kwa weledi.
4. Waombaji wanatakiwa kufika ofisi ya **Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda** kuchukua fomu ya maombi ya ujenzi wa vibanda kuanzia tarehe 25/03/2024, mwisho wa kuchukua fomu ni tarehe 02/04/2024

5. Maombi yote yawasilishwe ofisi ya **Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda** tarehe 10/04/2024 saa nne asubuhi. Maombi yawasilishwe yakiwa yamefungwa katika bahasha yenye gundi kali na ndani ya bahasha kuwe na **fomu itakayo onyesha gharama za uwekezaji, idadi ya vibanda ulivyo omba, muda wa uwekezaji** na viambata mbalimbali kwa mujibu wa sifa zilizoainishwa.
6. Waombaji wote wanatakiwa kuwepo wakati wa ufunguzi wa zabuni.
7. **Waombaji wanatakiwa kujaza fomu kwa kila kipengele kilicho ainishwa kwa usahihi na kuambatanisha nyaraka zote Muhimu kwa mujibu wa tangazo hili; kushindwa kufanya hivyo ni kigezo cha kukosa sifa ya kujadiliwa.**

Wako katika utumishi wa umma



MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA

MKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA MPANDA
S.L.P. 216
MPANDA-KATAVI